Wizara ya Habari, Utamaduni,
Sanaa na Michezo
Idara ya Habari-MAELEZO

Maelezo

Dodoma, 13 Julai, 2026

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MAKALA YA BBC

Serikali imesikitishwa na makala iliyochapishwa leo tarehe 13 Julai, 2026 na Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) kupitia kipindi chake cha "BBC Africa Eye" ambayo imebeba maudhui ya upande mmoja, yaliyokosa ushahidi thabiti, yenye upungufu wa taarifa muhimu na yenye mwelekeo wa kuichafua heshima ya Tanzania Kimataifa.

Chombo cha habari cha BBC kimeendelea na mwenendo wake wa kuitangaza vibaya Tanzania kwa tuhuma nzito pasipo kutoa nafasi ya Serikali kujibu kama kinavyopaswa kufanya kwa mujibu taaluma ya uandishi wa habari licha ya Serikali kuwa tayari kutoa ushirikiano kama ambavyo kimefanya katika makala hii ambapo kilikataa kutoa nafasi kwa viongozi wawili wa upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kufuatia upungufu huu wa kiweledi ambao haukupaswa na hautegemewi kufanywa na chombo cha habari kinachotarajiwa kuwa na heshima kama BBC, Serikali ya Tanzania inachukulia kwa uzito mwelekeo wa maudhui ya BBC dhidi ya Tanzania na inafanya tathmini ya kina ya makala hiyo.

Mara tathmini hiyo itakapokamilika, Serikali itachukua hatua zenye lengo la kulinda uhuru, heshima na usalama wa nchi dhidi ya mashambulizi ambayo yanafanywa kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii ikiwa ni pamoja na kutoa ufafanuzi wa upotoshaji na uchochezi wa makusudi uliojitokeza katika makala ya BBC.

Serikali inatoa wito kwa Watanzania wote kuwa makini na chokochoko zinazofanywa dhidi ya Tanzania kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, na inapenda kuwahakikishia wananchi wote kuwa itaendelea kusimamia misingi yote ya kudumisha amani, umoja na mshikamano wa Watanzania wote huku ikitekeleza afua mbalimbali za kukabiliana na changamoto zinazojitokeza kisiasa, kiuchumi na kijamii kwa lengo la kuimarisha ustawi wa jamii.

Gerson Msigwa
Katibu Mkuu, Wizara ya Habari, Utamaduni,Sanaa na Michezo
na Msemaji Mkuu wa Serikali